



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA YA KUSITISHWA USAJILI KWA WANAFUNZI WALIOSOMA MAFUNZO YA UUGUZI NA UKUNGA KWA NJIA YA MASAFI

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa Mujibu wa Sheria ya mwaka 2010 pamoja na Kanuni zake lina wajibu wa kulinda na kuhifadhi usalama wa afya ya umma. Ili kutimiza adhima hii, Baraza kwa Mujibu wa Kifungu cha 6(a), (d-f) limeandaa Miongozo inayoelekeza viwango vya usimamizi wa mafunzo, pamoja na kuendesha mtihani wa leseni kwa Wataaluma waliofuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada.

Baraza kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi sasa limekuwa likiorodhesha wahitimu waliosoma na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga kwa njia ya masafa (*Distance learning*) ambapo mafunzo hayo yalisitishwa rasmi mnamo na Wizara ya Afya mwaka 2012.

Napenda kuwajulisha kuwa, Baraza katika kikao chake cha **208** kilichofanyika tarehe **13/1/2022** kilifikia maamuzi ya wahitimu wote waliyosoma kwa program ya masafa (*Distance learning*) kwa ngazi ya **astashahada** ambayo ilianza **2006** na kuhitimishwa **2012**, wawe wamekamilisha taratibu za kuorodheshwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kwa Mujibu wa Vigezo. Uorodheshwaji kwa wahitimu wa program hii utafikia mwisho ifikapo **mwezi Julai, 2023**.

Aidha, wahitimu ambao walishaanza na wanaendelea kufanya mitihani wanaelekezwa kuendelea kufanya mitihani kwa Mujibu wa Mwongozo uliowekwa, kama maandalizi ya kuorodheshwa.

Nawatakia ushirikiano mwema.

Amama
Agnes Mtawa
MSAJILI
22/03/2023